

JARIDA LA MAENDELEO YA JAMII HALMASHAURI YA TARIME



MIKOPO YA 10 % KUANZIA 2012 MPAKA 2023

MWAKA	IDADI YA VIKUNDI			JUMLA	MKOPO TOLEWA			JUMLA
	V	W	WWU		VIJANA	WANAWAKE	WENYEULEMA-VU	
2012-2013	5	10	-	15	5,000,000	10,000,000	-	15,000,000
2014-2015	16	13	0	29	29,000,000	27,500,000	0	56,500,000
2015-2016	58	63	1	122	102,000,000	107,500,000	2,500,000	212,000,000
2016-2017	23	46	1	70	86,500,000	130,500,000	2,500,000	219,500,000
2017-2018	26	41	1	68	117,000,000	157,500,000	3,000,000	277,500,000
2018-2019	50	67	5	122	211,500,000	317,500,000	21,000,000	550,000,000
2019-2020	35	90	6	131	234,500,000	514,500,000	28,000,000	777,000,000
2020-2021	40	88	9	137	254,500,000	562,500,000	35,000,000	852,000,000
2021-2022	41	87	9	137	491,381,359	689,500,000	53,500,000	1,234,381,359
2022-2023	37	52	28	117	294,000,000	574,000,000	194,234,416.38	1,062,234,416.38
JUMLA	331	557	60	948	889,381,359	3,091,000,000	339,734,416	5,256,115,775



PICHA JENGO LA UKATILI WA KIJINSIA HOSPITALI YA NYAMWAGA

MAPAMBANO DHIDI YA UKATILI WA KIJINSIA (GBV)

UJENZI JENGO LA UKATILI WA KIJINSIA

Mradi wa jengo la ukatili wa kijinsia (GBVs) linalopatikana katika kata ya nyamwaga katika hospitali ya halmashauri ya tarime , ni mradi uliofadhiliwa na shirika la UNFP ili kupunguza na kutoa huduma za ukatili wa kijinsia katika halmashauri ya tarime .



PICHANI NI GARI YA UKATILI WA KIJINSIA KWA UFADHILI WA SHIRIKA LA UNFPA

Katika kuhakikisha huduma zinawafikia wahanga wa ukatili wa kijinsia , idara ya maendeleo ya jamii imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali , kuleta motisha na kusaidia vifaa ambavyo vitasaidia katika mapambano ya ukatili wa kijinsia

Shirika ya UNFP limeonyesha ushiriki wake kwa kutoa gari lenye thamani ta tsh gari ambalo litahudumia maswala yote ya ukatili wa kijinsia katika halmashauri ya tarime , hata hivyo idara ya maendeleo ya jamii imeendelea na jitihada za kupambana na ukatili wa kijinsia kwa kuendelea kutoa elimu katika jamii na makundi mbali ya akina mama , wazee wa kimila na wanafunzi kupinga na kutoa taarifa za ukatili wa kijinsia ikiwa ni Pamoja na matukio ya ukeketaji, Pamoja na hayo kamati za MTAKUWWA (Mpango mkakati wa kitaifa wa kupunguza na kutokomeza ukatili wa kijinsia dhidi ya wanawake na mtoto) zimeundwa na kuwezesha kwa mafunzo ili



MAFUNZO YA UKATILI WA KIJINSIA KATA YA NYAMWAGA

Idara ya maendeleo ya jamii imeendelea kutoa elimu juu ya ukatili wa kijinsia katika maeneo tofautitofauti ya halmashauri ya tarime ikiwa ni moja ya jitihada za kuhakikisha kuwa swala la ukatili wa kijinsia haswa ukeketaji wa watoto unaisha katika halmashauri ya tarime , hata hivyo idara imendelea na uwezeshaji wa kamati za MTAKUWWA kwa kuzipa mafunzo ya namna ya kufanya kazi katika ngazi ya kata na vijiji.



WANAFUNZI WA SHULE YA SEKONDARI INCHAGE WAKIPATIWA ELIMU YA MAAMBUKIZI YA VVU

Katika jitihada za kupunguza maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi katika maeneo ambayo yamepitiwa na mradi wa barabara idara ya maendeleo imeendelea kushirikiana na shirika nyanza road work company ltd kuendelea kutoa elimu ya maambukizi ya VVU kwa makundi mbalimbali ya wanafunzi , wanawake na vijana ili kukumbusha namna bora ya kujikinga na maambukizi.



PICHANI NI AKINA MAMA KATA YA NYAMWAGA WAKIPATA ELIMU YA MAAMBUKIZI YA VVU

Katika kuendeleza dhamira ya kupunguza maambukizi mapya ya VVU idara imeendeleza jitihada za kutoa elimu katika makundi mbalimbali ili kuzuia maambukizi mapya ya VVU